BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2018

## 621 KISWAHILI

# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

## TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2018

## 621 KISWAHILI

*Kimechapwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P  2624, Dar es Salaam,
Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2018**

Haki zote zimehifadhiwa.

**YALIYOMO**

DIBAJI .................... iv
1.0 UTANGULIZI .................... 1
2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI .................... 2
2.1 SEHEMU A: MASWALI YANAYOHITAJI MAJIBU MAFUPI KUTOKA MADA ZA TAALUMA NA UFUNDISHAJI. .................... 2
2.1.1 Swali la 1: Stadi za Lugha .................... 2
2.1.2 Swali la 2: Fasihi Simulizi .................... 5
2.1.3 Swali la 3: Stadi za Lugha .................... 7
2.1.4 Swali la 4: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili .................... 10
2.1.5 Swali la 5: Fasihi Simulizi .................... 13
2.1.6 Swali la 6: Maandalizi ya Ufundishaji .................... 16
2.1.7 Swali la 7: Utungaji .................... 18
2.1.8 Swali la 8:Sarufi .................... 20
2.1.9 Swali la 9. Upimaji .................... 23
2.1.10 Swali la 10: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili .................... 26
2.2 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA YANAYOHUSU MADA ZA TAALUMA .................... 29
2.2.1 Swali la 11:Ufahamu .................... 29
2.2.2 Swali la 12: Utungaji .................... 32
2.2.3 Swali la 13: Fasihi Simulizi .................... 36
2.3 SEHEMU C: MASWALI YA INSHA YANAYOHUSU MADA ZA UFUNDISHAJI .................... 39
2.3.1 Swali la 14: Upimaji .................... 39
2.3.2 Swali la 15: Zana za Kufundishia na Kujifunzia Soma la Kiswahili .................... 44
2.3.3 Swali la 16: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili .................... 48
3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA .................... 52
4.0 HITIMISHO .................... 53
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO .................... 54
KIAMBATISHO A .................... 55
KIAMBATISHO B .................... 56

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa kitabu hiki kinachohusu taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu Ualimu Daraja la A kwa somo la Kiswahili.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho inayoonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa maarifa ambayo walipata au walishindwa kupata walipokuwa katika mafunzo ya Ualimu.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri, vibaya au kwa kiwango cha wastani katika mtihani huu. Taarifa hii inaonesha baadhi ya sababu zilizowafanya watahiniwa wengi kufanya vizuri, kama vile kuelewa maelekezo na matakwa ya swali, kuwa na maarifa na ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha na kuwa na uelewa wa mada mbalimbali zilizotahiniwa. Aidha, sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutokufanya vizuri zimefafanuliwa pia. Sababu hizo ni kama vile kutokuelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa watahiniwa kujieleza kwa kutumia lugha fasaha na udhaifu katika kuelewa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili.

Taarifa hii itawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule na vyuo, wakufunzi na walimu tarajali kupata mbinu stahiki zitakazosaidia kuboresha kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika mitihani ijayo inayotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania linakaribisha maoni na mapendekezo kutoka kwa wakufunzi, walimu tarajali na umma kwa ujumla, ambayo yatatumika katika kuboresha taarifa za watahiniwa zitakazofuata.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru maafisa mitihani, wakufunzi wa somo na wengine wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii. Tunapenda pia kutoa shukrani zetu za pekee kwa wafanyakazi wa Idara ya Utafiti na Tathmini na Huduma za Kompyuta kwa kushiriki katika uchambuzi wa data zilizotumika katika taarifa hii.

Dr Charles Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Lengo la taarifa hii ni kuchambua viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika mtihani wa Ualimu Daraja la A kwa somo la Kiswahili uliofanyika tarehe 08 Mei, 2018. Mtihani huu ulikuwa na maswali 16 yaliyogawanywa katika sehemu A, B, na C kwa kuzingatia mada za *Taaluma* na *Ufundishaji*.

Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ambapo kila swali lilikuwa na alama nne (4). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii. Jumla ya alama katika sehemu hii ilikuwa ni arobaini (40). Maswali ya sehemu hii yalikuwa ya mchanganyiko wa mada zinazohusu *Taaluma* na *Ufundishaji*.

Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) yanayohusu mada za *Taaluma*. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) tu na kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15). Hivyo, jumla ya alama katika sehemu hii ilikuwa ni thelathini (30).

Sehemu C ilikuwa na maswali matatu (3) yanayohusu mada za *Ufundishaji*. Katika sehemu hii mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) na kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15). Hivyo, jumla ya alama za sehemu hii zilikuwa ni thelathini (30).

Kwa ujumla, mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali kumi na manne (14) kati ya maswali kumi na sita (16).

Mtihani huu ulikuwa na viwango vitatu vya kufaulu ambavyo ni kiwango kizuri kuanzia alama 70 hadi 100, kiwango cha wastani kuanzia alama 40 hadi 69 na kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 39.

Watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani wa 621 Kiswahili kwa mwaka 2018 walikuwa 4,954. Kati ya hao, watahiniwa waliofanya mtihani ni 4,897 ilihali watahiniwa 57 hawakufanya mtihani. Miongoni mwa watahiniwa waliofanya mtihani, waliofaulu kwa daraja A hadi D ni 4,866 sawa na asilimia 99.79 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Aidha watahiniwa 10 sawa na asilimia 0.2 walipata daraja F. Kiwango hiki cha kufaulu ni kizuri. Sehemu inayofuata ni tathmini ya kila swali ambapo viwango vya kufaulu vya watahiniwa vinaonekana bayana.

## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Sehemu hii inahusu uchambuzi wa kina wa kila swali na majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kuonesha maswali yaliyofanywa vizuri, wastani na yale yaliyofanywa vibaya. Aidha, sababu za kufaulu kwa kila kiwango yaani cha juu, wastani na cha chini kwa watahiniwa zimeelezwa bayana kwa kila swali. Vilevile, sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya vizuri na vibaya katika kila swali zimeambatanishwa ili kuonesha majibu yaliyotakiwa kutolewa kwa kila swali na majibu ambayo hayakutakiwa. Aidha, sampuli hizo zitasaidia kudhihirisha maelezo ya uchambuzi huu.


Swali litaelezwa kwamba limejibiwa vizuri ikiwa theluthi mbili (2/3) na zaidi ya watahiniwa wamelijibu vizuri inavyotakiwa na kupata alama za juu na litaelezwa kuwa limejibiwa vibaya ikiwa ni theluthi (1/3) ya watahiniwa waliolijibu vizuri. Aidha, swali litaelezwa limejibiwa kwa wastani ikiwa idadi ya watahiniwa waliojibu vizuri inazidi theluthi moja (1/3) na haikuzidi theluthi mbili (2/3).

## 2.1 SEHEMU A: MASWALI YANAYOHITAJI MAJIBU MAFUPI KUTOKA MADA ZA TAALUMA NA UFUNDISHAJI.

### 2.1.1 Swali la 1: Stadi za Lugha

Swali hili limetoka katika mada za *Taaluma* hususan mada kuu ya *Stadi za Lugha*. Swali lililenga kupima maarifa ya watahiniwa juu ya mawasiliano. Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze mambo manne ya kuzingatia ili kuwapo mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji.


Swali hili lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani na lilikuwa ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Kati yao, asilimia 79.3 walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati namba 1**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 52.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hawa walipata alama za juu kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Mawasiliano* na walielewa matakwa ya swali. Hawa waliweza kubainisha mambo manne ya kuzingatia ili kuwepo mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji ambayo ni *usikivu, mada itakayozungumzwa, mahali na uhusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji*. Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwa kuwa majibu yake yalikidhi matakwa ya swali.

**Kielelezo 1.1**



1. i) Usikivu; ili mawasiliano yaweze kuwepo kati ya mzungumzaji na msikilizaji hakuna budi kuwepo kwa usikivu ili waweze kusikiliza juu ya kile kinachozungumzwa.
ii) Mada itakayo zungumzwa; ni muhimu kuwepo kwa mada au jambo litakalo kuwa linazungumzwa au linalotolewa ufafanuzi.
iii) Mahali; sehemu ambayo mazungumzo hayo yatafanyika na sehemu hiyo iendane na aina ya mazungumzo.
iv) Uhusiano baina ya mzungumzaji na msikilizaji; kwa mfano mazungumzo ya mtoto na mzazi au mazungumzo ya mshawishi na mshawishiwa.

**Kielelezo 1.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwa kubainisha mambo manne ya kuzingatia ili kuwepo mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji.

Asilimia 27.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kutokana na kutokuandika majibu yanayojitosheleza vizuri. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa walibainisha mambo mawili badala ya mambo manne kama swali lilivyotaka.

Aidha, asilimia 20.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi ya watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa juu ya mada ya *Mawasiliano* na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali. Kielelezo 1.2 ni sampuli ya mtahiniwa aliyepata alama 0 kwa kuwa aliandika majibu ambayo ni kinyume kabisa na matakwa ya swali.

**Kielelezo 1.2**




1. Mambo ya kuzingatia ili kuwepo na Mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji ni i) Lafudhi
ii) Mkazo
iii) Kiimbo
iv) Kasi

Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kushindwa kubainisha mambo ya kuzingatia ili kuwepo mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji.

### 2.1.2 Swali la 2: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada za *Taaluma* hususan mada kuu ya *Fasihi Simulizi*. Swali hili lililenga kupima uelewa wa watahiniwa juu ya vitendawili ambapo lilimtaka mtahiniwa kueleza sifa nne za vitendawili.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 82.9 walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 2**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 68.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia alama 3 hadi 4 kwa sababu waliweza kueleza kwa usahihi sifa nne za vitendawili. Sifa zilizoelezwa ni pamoja na *vitendawili huhusisha watu wawili, huwa na swali na jibu fupi, huwa na maana ya mficho na huzungumzwa na kila rika*. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada hii ya vitendawili na walielewa matakwa ya swali. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama 4 kwa kuwa aliweza kueleza sifa nne za vitendawili.

**Kielelezo 2.1**


2. Sifa nne za vitendawili
i) vitendawili huusisha watu wawili tu Muulizaji na mteguaji.
ii) Vitendawili huwa na swali na jibu fupi tu.
iii) vitendawili huwa na maana ya mficho.
iv) vitendawili huzungumzwa na kila rika.

**Kielelezo 2.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza vizuri sifa nne za vitendawili.

Asilimia 14.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani 1.5 hadi 2.5. Watahiniwa hawa walipata alama za wastani kwa sababu hawakuzingatia matakwa ya swali na badala yake sifa walizozitaja hazikufika nne na wengine walirudia kutaja sifa moja mara mbili. Pia, baadhi yao walichanganya sifa za vitendawili na umuhimu wa vitendawili. Kutokana na hali hiyo walipata alama za wastani.

Vilevile, asilimia 16.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kutokana na kutokuwa na uelewa juu ya mada ya *Vitendawili*. Aidha, baadhi ya watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali. Baadhi yao walieleza umuhimu au faida za vitendawili badala ya kueleza sifa za vitendawili. Watahiniwa hawa walieleza umuhimu wa vitendawili kama *kurithisha kutoka enzi, kuelimisha jamii, kuonya na kukuza lugha* badala ya sifa za vitendawili ambazo ni *kuwa na swali fupi, kuwa na maana ya mficho, kuzungumzwa na kila rika na kuhusisha watu wawili*.Kielelezo 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama 0 kutokana na kutokuelewa matakwa ya swali.

**Kielelezo 2.2**


Q2 i) Hurithisha kutoka enzi
ii) Huelimisha jamii
iii) Huonya
iv) Hukuza lugha


Kielelezo 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza sifa za vitendawili. Majibu yake yalijikita katika umuhimu wa vitendawili badala ya sifa za vitendawili.

### 2.1.3 Swali la 3: Stadi za Lugha

Swali lilitoka katika mada za *Taaluma* hususan mada kuu ya *Stadi za Lugha.* Swali hili lililenga kupima maarifa ya watahiniwa katika uwanja wa utungaji ambapo lilimtaka mtahiniwa kutaja kwa kifupi mambo manne ya kuzingatia katika utungaji wa mazungumzo.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani yaani asilimia 100 na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 83.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri na kupata alama za wastani na


zaidi. Chati namba 3 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati namba 3**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 61.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hawa waliweza kutaja kwa usahihi mambo manne ya kuzingatia katika utungaji wa mazumngumzo kwa sababu walielewa vizuri mada ya *Utungaji*, pamoja na matakwa ya swali. Mambo hayo ni *kuwe na jambo la kujieleza, kuwepo na kusudio la kuzungumza, kuwa na ari ya kujieleza na kuwa na mpangilio mzuri wa mawazo.* Kuthibitisha hayo, kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama 4.

**Kielelezo 3.1**




3. Mambo manne ya kuzingatia katika utungaji wa mazungumzo ni
i. Kuwe na jambo la kujieleza.
ii. Kuwepo na kusudi au sababu ya utungaji huo.
iii. Kuwepo na hamasa au ari ya kujieleza au utungaji.
iv. Kuwepo na mpangilio mzuri wa maneno kimantiki.

**Kielelezo 3.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi mambo manne ya kuzingatia katika utungaji wa mazungumzo.

Vilevile, asilimia 21.4 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwa sababu hawakuwa na ujuzi wa kutosha wa mada ya *Utungaji wa Mazungumzo*. Hali hiyo, ilisababisha watahiniwa hawa kushindwa kutaja kikamilifu mambo manne ya kuzingatia katika utungaji wa mazungumzo. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walichanganya hatua za utungaji wa mazungumzo na mambo ya kuzingatia katika utungaji wa mazungumzo.

Aidha, asilimia 16.9 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Inaonekana baadhi ya watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa juu ya mada ya *Utungaji wa Mazungumzo* na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliopata alama hafifu waliandika majibu ambayo hayaendani kabisa na swali. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali na kupata alama hafifu.

**Kielelezo 3.2**



3 (i) kutazama uwezo wa kutazamana na watu ili kuweza
kusoma mazungumzo yaliyokusudiwa.
(ii) kuzingatia mtindo wa Lugha utakaotumika katika
mazungumzo hayo.
(iii) Viungo vya mwili mfano kichwa, midomo huweza
kuonyesha ishara katika mazungumzo.
(iv) Usikubali kutamka maneno magumu ili kuweza
kueleweka pande zote.

**Kielelezo 3.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubaini matakwa ya swali. Mtahiniwa huyu aliandika majibu ambayo ni kinyume kabisa na matakwa ya swali.

### 2.1.4 Swali la 4: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada za *Ufundishaji* na katika mada kuu ya *Mbinu Anuai za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuorodhesha mbinu nne atakazotumia mwalimu kufundishia ufupisho katika somo la Kiswahili.


Swali hili lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani na ni miongoni mwa maswali yaliyofanywa vizuri. Asilimia 75.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Watahiniwa hawa walielewa vizuri mada ya *Mbinu za Ufundishaji* ambayo ndio msingi wa utaalamu wao. Chati namba 4 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati Namba 4**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia.

Asilimia 61.5 walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili* hivyo, waliweza kuorodhesha kwa usahihi mbinu nne za kufundishia ufupisho ambazo ni *onesho mbinu, maswali na majibu, majadiliano na matembezi ya galare*. Kielelezo 4.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote 4.

**Kielelezo 4.1**



04 Mbinu za kufundisha ufupisho katika somo la kiswahili

i) Onesho mbinu

ii) Maswali na majibu


iii) Majadiliano

iv) Matembezi ya galari

**Kielelezo 4.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeorodhesha kwa usahihi mbinu nne za kufundishia ufupisho.

Aidha, asilimia 24.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili hawakujibu vizuri hivyo walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi ya watahiniwa hawa, hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mbinu za kufundishia ufupisho. Aidha, wengine hawakuelewa matakwa ya swali kwani badala ya kuorodhesha mbinu za kufundishia ufupisho waliorodhesha hatua za kufanya ufupisho. Kadhalika wengine waliorodhesha umuhimu wa ufupisho katika lugha. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

**Kielelezo 4.2**


4. (i) Kusoma kwa makini Habari tuliyo
pewa kufanyia Ufupisho
(ii) Kurudia kusoma Habari hiyo kwa ma
ra mbili au tatu.
(iii) Kubaini Mawazo Makuu na ala
ma za Uandishi
(iv) Kuandika Ufupisho huo kwa kufua
ta taratibu na Sheria za Uandishi wa Ufupi
sho.


**Kielelezo 4.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubaini matakwa ya swali. Mtahiniwa huyu aliorodhesha hatua za kufanya ufupisho badala ya mbinu za kufundishia ufupisho.

Pia, asilimia 14.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwa kuwa hawakujibu swali hili kikamilifu. Baadhi yao hawakutimiza matakwa ya swali kwani walitaja mbinu chache ilihali swali lilitaka mbinu nne. Pia, wengine walichanganya mbinu za kufundishia ufupisho na hatua za kufanya ufupisho.

### 2.1.5 Swali la 5: Fasihi Simulizi

Swali hili limetoka katika mada za *Taaluma* na katika mada kuu ya *Fasihi Simulizi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua kwa kifupi faida nne za fasihi simulizi katika jamii.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani yaani asilimia 100. Swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo yalijibiwa vizuri ambapo asilimia 90.8 walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 5 inaonesha viwango vya kufaulu kiasilimia.




**Chati Namba 5**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Kati ya watahiniwa waliojibu swali hili, asilimia 56.0 walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hawa waliweza kuchambua faida nne za fasihi simulizi kwa usahihi ambazo ni *kuburudisha jamii, kuelimisha, kurithisha amali za jamii na kukosoa au kuonya jamii kwa sababu walielewa matakwa ya swali*. Kielelezo 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwa kuweza kuchambua kwa usahihi na kwa mifano faida nne za fasihi simulizi.

**Kielelezo 5.1**

5 i) fasihi simulizi huburudisha; katika fa-
sihi mtu huweza kuburudika kwa vicheke-
sho na hadithi za utani ambavyo huwa
ndani ya fasihi simulizi.

ii) Fasihi simulizi huelimisha jamii; Hii
hutokana na baadhi ya vipera vyake ka-
ma hadithi ambavyo ujumbe wake hutoa
elimu kwenye jamii mfano Hekaya

iii) fasihi simulizi hurithisha amali za
jamii; kwa kupitia fasihi jamii huweza ku
jifunza mambo ya kale na kuweza kutunza
mila na tamaduni zao mfano kusalimia

iv) fasihi simulizi hukosoa na kuonya ja-
mii; kwa kupitia vipera vyake mfano
mashairi, semi huweza kutoa ujumbe
unaoweza kukosoa na kuonya jamii kuto
kana na mwenendo mbaya wa jamii.


**Kielelezo 5.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.

Vilevile, asilimia 35.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwa sababu hawakuzingatia matakwa ya swali. Baadhi hawakuweza kupata alama zote nne (4) kwa sababu baadhi ya mambo waliyoyachambua sio faida za fasihi simulizi.

Hali kadhalika, watahiniwa wachache sana ambao ni asilimia 8.8 walipata alama hafifu kati ya 0 hadi 1.5 kwa sababu hawakuwa na uelewa juu ya mada ya *Fasihi Simulizi* na vile vile hawakuelewa matakwa ya swali. Kutokana na hali hiyo, watahiniwa hawa walishindwa kujibu swali kwa usahihi. Kwa mfano, baadhi yao walichambua sifa za fasihi simulizi badala ya faida za fasihi simulizi. Sifa walizochambua ni *huwasilishwa kwa njia ya mdomo, haibagui, ujumbe wa awali huweza kubadilika na haina gharama badala ya kuchambua faida ambazo ni kuburudisha jamii, kuelimisha, kurithisha amali za jamii na kukosoa au kuonya jamii*. Aidha wengine walichambua tanzu za fasihi simulizi badala ya faida za fasihi simulizi. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya

majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kushindwa kuchambua faida nne za fasihi simulizi na kupata alama 0.

**Kielelezo 5.2**



5. i/ Huwasilishwa kwa njia ya mdomo
ii/ Haibagui yaani kumfikia ujumbe
wake anayejua kusoma na asiye
jua kusoma
iii/ Ujumbe wa awali unaweza kuba
dilika
iv/ Haina gharama.

**Kielelezo 5.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

### 2.1.6 Swali la 6: Maandalizi ya Ufundishaji

Swali lilitoka katika mada za *Ufundishaji* na katika mada kuu ya *Maandalizi ya Ufundishaji.* Swali lililenga kupima maarifa au uelewa wa mtahiniwa juu ya mtaala na vifaa vyake. Swali lilimtaka mwanafunzi kutaja vifaa vinne (4) vya mtaala wa somo la Kiswahili shule za msingi.


Swali lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani yaani asilimia 100. Swali hili lilifanywa vizuri ambapo asilimia 98 walipata alama za wastani na zaidi. Viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika swali hili vimeoneshwa katika chati namba 6.




**Chati Namba 6:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 94.1 kati ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya vifaa vya mtaala. Watahiniwa wa kundi hili waliweza kutaja kwa usahihi vifaa vinne vya mtaala wa somo la Kiswahili shule za msingi. Kwa mfano vifaa walivyotaja ni *muhtasari wa somo la Kiswahili, kiongozi cha mwalimu, kitabu cha kiada na kitabu cha ziada/rejea*. Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwani aliweza kutaja kwa usahihi vifaa vinne vya mtaala wa somo la Kiswahili shule za msingi.

**Kielelezo 6.1**




| | | |
|---|---|---|
| 6 | Vifaa u vya mtaala wa somo la Kiswahili | |
| | i) Muhtasari wa somo la Kiswahili | |
| | ii) Kiongozi cha mwalimu | |
| | iii) Kitabu cha kiada | |
| | iv) Kitabu cha ziada | |

**Kielelezo 6.1** kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuzingatia matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa wachache ambao ni asilimia 3.9 walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Baadhi yao walishindwa kutimiza kikamilifu matakwa ya swali kwa kutaja sifa pungufu ya zile zilizohitajika katika swali kutokana na uelewa mdogo juu ya mada ya *Vifaa vya Mtaala*. Pia, wengine walichanganya vifaa vya mtaala na vifaa vya kufundishia.

Vilevile, asilimia 2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya vifaa vya mtaala. Baadhi yao, walichanganya vifaa vya kufundishia na vifaa vya mtaala na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama 0 kwa kushindwa kutaja vifaa vya mtaala.

**Kielelezo 6.2**




| | | |
|---|---|---|
| 6 | (i) Malengo | |
| | (ii) Maudhui | |
| | (iii) Vifaa na mbinu au njia za kufundishia | |
| | (iv) Tathimini | |

**Kielelezo 6.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

### 2.1.7 Swali la 7: Utungaji

Swali hili lilitoka katika mada za *Taaluma* na katika mada kuu ya *Utungaji*. Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa juu ya mashairi ambapo mtahiniwa alitakiwa kuainisha sifa nne za shairi la kimapokeo.


Swali hili lilijibiwa na asilimia 99.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Kati yao, asilimia 70.8 walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 7 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 7**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Aidha, asilimia 36.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hawa walifaulu vizuri kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Ushairi* na walizingatia matakwa ya swali. Watahiniwa hawa waliweza kuainisha sifa nne za shairi la kimapokeo ambazo ni *lazima liimbike, liwe na urari wa vina na mizani, mishororo minne katika beti na liwe na mizani kumi na sita*. Kielelezo 7.1 ni miongoni mwa sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu vizuri kulingana na matakwa ya swali na kupata alama 4.

**Kielelezo 7.1**


7. Sifa za shairi la kimapokeo.

i/ shairi liimbike
ii/ Shairi liwe na beti lenye mishororo minne
iii/ Shairi liwe na mizani kumi na sita (16)
iv/ shairi lizingatie urari wa vina na mizani

**Kielelezo 7.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeainisha kwa usahihi sifa nne za shairi la kimapokeo.

Hali kadhalika, asilimia 31.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Baadhi ya watahiniwa hawa walichanganya dhima za shairi la kimapokeo na sifa za shairi la kimapokeo.

Aidha, asilimia 31.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hawa walishindwa kuainisha sifa nne za shairi la kimapokeo kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Utungaji*. Baadhi yao waliandika sifa za shairi la kisasa badala ya sifa za shairi la kimapokeo na wengine walichanganya dhima za shairi na sifa za shairi. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama 0.

**Kielelezo 7.2**


| | | |
|---|---|---|
| 7. | i/ Shairi la Kimapokeo huwa na beti nne | |
| | ii/ Shairi la Kimapokeo halina ulazima wa vina Kufa | |
| | nana na mizani | |
| | iii/ Shairi la Kimapokeo halina ufanano wa Kuwa | |
| | na Kituo tamali. | |
| | iv/ Shairi la Kimapokeo halina upungufu wa silabi | |
| | Kumi na sita Kila mshororo | |

**Kielelezo 7.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeainisha sifa nne za shairi la kisasa badala ya shairi la kimapokeo.

### 2.1.8 Swali la 8:Sarufi

Swali hili lilitoka katika mada za *Taaluma* na katika mada kuu ya *Sarufi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha aina nne za vielezi na kisha kutunga sentensi moja kwa kila aina.


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani yaani asilimia 100. Asilimia 80.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 8 inaonesha viwango vya kufaulu kiasilimia.




**Chati Namba 8**. Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 48.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hawa walifanya vizuri kwa sababu walikuwa na uelewa mpana juu ya mada ya *Sarufi* hususan kipengele cha uainishaji wa maneno na waliweza kuzingatia matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliweza kuainisha aina nne za vielezi pamoja na kubainisha kielezi hicho katika sentensi walizotunga. Aina nne za vielezi vilivyobainishwa ni *vielezi vya namna, vielezi vya idadi, vielezi vya mahali na vielezi vya wakati.* Kielelezo 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kulingana na matakwa ya swali na kupata alama 4.

**Kielelezo 8.1**



8 (i) vielezi vya namna
sentensi: Wanyama wale wanatembea pole pole
E
(ii) vielezi vya idadi
sentensi: Yeye huja nyumbani mara kwa mara
E
(iii) vielezi vya mahali
sentensi: Wanafunzi wanacheza mpira uwanjani
E
(iv) vielezi vya wakati
sentensi: Shangazi alijifungua mtoto mwaka jana
E

> **Kielelezo 8.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha kwa usahihi aina nne za vielezi na kukibainisha katika kila sentensi aliyotunga.

Aidha, asilimia 31.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia alama 2 hadi 2.5 kwa sababu ya kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Sarufi* hususan kipengele cha aina za maneno. Baadhi yao walichanganya aina za maneno na wengine walishindwa kutimiza matakwa ya swali kama vile, kutunga sentensi kwa kila aina ya kielezi alichokibainisha. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliweza kutaja aina ya kielezi lakini wakashindwa kuonesha kielezi hicho katika sentensi.

Hali kadhalika, asilimia 20.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa juu mada ya *Sarufi* hususan mada ndogo ya aina za maneno hivyo walijibu kinyume na matakwa ya swali kwa kuandika aina za vielezi ambazo ni *kielezi nomino, kielezi kitenzi, kielezi kikuu na kielezi kiwakilishi* badala ya *vielezi vya namna, vielezi vya idadi, vielezi vya mahali na vielezi vya wakati*. Kielelezo 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa wa kundi hili ambaye alipata alama 0.

**Kielelezo 8.2**



7. i) Kielezi kitenzi
- Kabatini kuna vyombo vingi.
ii) Kielezi nomino
- Mama anaenda shambani.
iii) Kielezi ~~kivumishi~~ kiwakilishi
- Yeye huenda kazini kila siku.
iv) Kielezi kitu
- Nimemkuta akicheza uwanjani.

**Kielelezo 8.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika majibu ambayo siyo sahihi kwa sababu ya kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya aina za maneno.

### 2.1.9 Swali la 9. Upimaji

Swali lilitoka katika mada za *Ufundishaji* na katika mada kuu ya *Upimaji*. Swali hili lililenga kupima uelewa wa watahiniwa juu ya mada ya *Upimaji* ambapo mtahiniwa alitakiwa kuorodhesha aina nne za maswali ya ufahamu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani yaani asilimia 100. Swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo yalipata ufaulu wa wastani ambapo asilimia 62 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 8 inaonesha viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 9**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 58.8 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Upimaji*.

Aidha, asilimia 38.0 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hawa walipata alama hafifu kwa sababu hawakuwa na uelewa juu ya mada ya *Upimaji* na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Mathalani baadhi ya watahiniwa walitunga maswali kwa mfano, *eleza faida za misitu katika jamii, eleza changamoto za biashara, fafanua matumizi ya mtaala na changanua vifaa vya muhtasari* badala ya kuandika aina za maswali ya ufahamu ambazo ni *maswali ya kueleza, kufafanua, kubainisha na kuchambua*. Na wengine walieleza aina za ufahamu. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama 0 kwa sababu alishindwa kuelewa matakwa ya swali.

**Kielelezo 9.1**

| | | |
|---|---|---|
| 9 (i) | Eleza faida za misitu katika jamii. | |
| (ii) | Ø Eleza changamoto za biashara. | |
| (iii) | Fafanua matumizi ya mtaala. | |
| (iv) | Changamua vifaa vya muhtasari. | |

**Kielelezo 9.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetunga maswali badala ya kuorodhesha aina za maswali ya ufahamu.

Hali kadhalika, watahiniwa wachache Sana ambao ni asilimia 3.2 kati ya watahiniwa waliofanya swali hili walijibu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa kuwa walielewa vizuri mada ya *Upimaji* na matakwa ya swali. Hawa waliweza kuorodhesha aina nne za maswali ya ufahamu ambazo ni *maswali ya kueleza, kufafanua, kubainisha na kuchambua*. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama 4.

**Kielelezo 9.2**


| | | |
|---|---|---|
| 9. | i). Maswali ya Kueleza. | |
| | mfano: Eleza mambo matatu ya kuzingatia wakati | |
| | wa kutunga mtihani. | |
| | | |
| | ii). Maswali ya Kufafanua. | |
| | mfano: Fafanua sehemu nne za utungaji wa | |
| | Insha. | |
| | | |
| | iii). Maswali ya Kubainisha. | |
| | mfano: Bainisha faida tano za maji. | |
| 9, | iv). Maswali ya Kuchambua. | |
| | mfano: Chambua mambo matano yanayosababisha | |
| | kuporomoka kwa maadili. | |

**Kielelezo 9.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeorodhesha aina nne za maswali kwa usahihi.

### 2.1.10 Swali la 10: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili

Swali hili lilitoka katika za mada za Ufundishaji hususan mada kuu ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili.* Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi mambo manne muhimu ya kuzingatia wakati wa kutumia mbinu ya ziara kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 99.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 79.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri na walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 10 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Namba 10**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 44.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kutokana na kutojibu kwa usahihi baadhi ya hoja. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili*.

Asilimia 34.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4 kwa kuwa walikuwa na ujuzi wa kutosha juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili*. Watahiniwa hawa waliweza kueleza kwa usahihi mambo ya kuzingatia wakati wa kutumia mbinu ya

ziara kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia. Mambo yaliyoelezwa ni *kuandaa mada ya kufanyia ziara, kutoa taarifa sehemu ambayo ziara itafanyika, kutoa taarifa kwa uongozi wa shule na kuandaa maswali ya kuongoza ujifunzaji katika ziara*. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama 4.

**Kielelezo 10.1**


10 Kueleza kwa ufupi mambo 4 muhimu ya kuzingatia katika kutumia mbinu ya ziara kwaajili ya kufundishia na kujifunzia

i) Kuandaa Mada.
Mwalimu anatakiwa kuandaa mada ambayo ataifanyia ziara ili wanafunzi wawele kujifunza.

ii) Kutoa taarifa sehemu ambayo anatala ka kwenda kufanya ziara na kwanda kuna kama malengo mahusi yaitafi kwa

iii) Kutoa taarifa kwa uongozi wa shule pamoja na wazazi walezi wa wanafunzi ambao ataendanao kufanya ziara.


iv) Kuandaa maswali ya kujifunza wanafunzi ambayo yatawasaidia kuuliza maswali ili kuepuka kuuliza maswali nje ya mada. na kuhakiki kuhusu usalama wa wanafunzi, chakula pamoja na malazi.

**Kielelezo 10.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa kifupi mambo manne muhimu ya kuzingatia anapotumia mbinu ya ziara kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.

Hata hivyo, asilimia 20.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, walieleza umuhimu wa ziara badala ya mambo ya kuzingatia anapotumia mbinu ya ziara katika kufundishia na kujifunzia

kinyume na matakwa ya swali. Walielezea umuhimu wa ziara kama *husaidia wanafunzi kutunza kumbukumbu, kuwa na uwezo wa kuelewa mambo waliojifunza, ufurahisha na humrahisishia mwalimu kazi* badala ya mambo ya kuzingatia inapotumika mbinu ya ziara ambayo ni *kuandaa mada ya kufanyia ziara, kutoa taarifa sehemu ambayo ziara itafanyika, kutoa taarifa kwa uongozi wa shule na kuandaa maswali ya kuongoza ujifunzaji katika ziara*. Kielelezo 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali na kupata alama 0.

**Kielelezo 10.2**


10 1/ Ziara humsaidia Mwanafunzi ~~Kumbu~~
Kutunza Kumbu kumbu ya Mambo haliyo yaon
a Kipindi akuwa Kwenye Ziara

2/ lefikirisha Mwanafunzi Kuwa na uwezo
Kuelewa Mambo halio Jifunza akuwa Kwenye
Ziara

3/ Ufurahisha Mwanafunzi na Kumfan
ya Mwanafunzi Kupata Maarifa Mapya

4/ Umurahisisha Kazi mwalimu Kipindi
anafundisha na Ziara hufanya Somo Kuhukuwa
Ka Zaidi


**Kielelezo 10.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza umuhimu wa mbinu ya ziara badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa kutumia mbinu ya ziara kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.

## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA YANAYOHUSU MADA ZA TAALUMA

### 2.2.1 Swali la 11:Ufahamu

Swali hili lilitoka katika mada kuu ya *Ufahamu* na lililenga kupima maarifa ya watahiniwa juu ya ufupisho. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza mambo matano ya kuzingatia wakati wa kufupisha habari.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 51.6 ya watahiniwa waliofanya mtihani na lilipata ufaulu wa kiwango cha wastani, ambapo asilimia 62.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 11 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati Namba 11**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Aidha, asilimia 54.7 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Baadhi ya watahiniwa hao hawakujibu kikamilifu kulingana na matakwa ya swali na wengine hawakufuata kanuni za uandishi wa insha. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walijibu swali hili kwa mtindo wa kuorodhesha hoja na hivyo kukosa alama za utangulizi, kuelezea hoja hizo, pamoja na hitimisho.

Vilevile, asilimia 37.5 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Ufupisho* na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kutokana na hali hiyo walishindwa kueleza

hatua zinazopaswa kufuatwa wakati wa kufupisha habari badala yake walieleza mambo ya jumla ya kuzingatia katika uandishi na wengine waliandika majibu ambayo hayahusiani na swali. Mambo ya jumla ya kuzingatia katika uandishi yaliyoelezewa ni *kiini cha habari yenyewe, matumizi sahihi ya alama, wahusika wa habari hiyo na lugha itakayotumika*. Aidha mtahiniwa alipaswa kueleza hatua zinazopaswa kufuatwa wakati wa kufupisha habari ambazo ni *kusoma habari kwa umakini, kudondoa/kubaini mawazo makuu, kuunganisha mawazo makuu kwa kutumia maneno yako mwenyewe, kupunguza maneno yasiyokuwa ya lazima na habari iliyofupishwa iwe (1/3) ya habari nzima*. Kielelezo 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

**Kielelezo 11.1**

11. Ufupisho wa habari ni kitendo cha kufupisha kifungu cha habari fulani bila kupoteza maana au kiini cha habari hiyo.

Ufupisho wa habari huzingatia mambo muhimu mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ya kuzingatia ni pamoja na :-

Kiini cha habari yenyewe. Hili ni jambo muhimu la kuzingatia pale unapofupisha habari ili usitoke nje ya maudhui ya habari yenyewe.

Matumizi sahihi ya alama za uandishi. Ili ufupisho wa habari uwe una manufaa ni lazima uzingatie matumizi sahihi ya alama za uandishi.

Wahusika au walengwa wa habari hiyo. Ili uweze kufanya ufupisho wa habari ni vyema utambue walengwa wa habari hiyo ni akina nani ili uweze kufikisha kwa urahisi.

Lugha iliyotumika na utakayotumia katika ufupisho wa habari. Jambo lingine la kuzingatia unapofupisha habari ni kuangalia lugha iliyotumika ili iweze kukupa nafasi ya kufupisha kwa urahisi.

Hivyo basi, unapofanya ufupisho wa habari fulani ni vyema kuzingatia mambo haya ili kutopoteza maana ya habari iliyokusudiwa.

**Kielelezo 11.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali kwa kueleza mambo ya jumla ya kuzingatia katika uandishi badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya ufupisho wa habari.

Watahiniwa wachache ambao ni asilimia 7.8 walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Ufupisho* kwa sababu waliweza kueleza mambo matano ya kuzingatia wakati wa kufupisha habari. Hali kadhalika, waliweza kuandika insha yenye mtiririko mzuri wa hoja kwa kufuata hatua zote za uandishi wa insha. Ili kuthibitisha haya, kielelezo 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kuzingatia kanuni za uandishi wa insha na kupata alama za juu.

**Kielelezo 11.2**

11 Ufupisho ni uchanganuzi na uchambuzi wa jambo alilosoma au alilosikiza mtu bila kupoteza kiini cha habari ya awali, kwa kudondoa mawazo makuu ya habari. Ili kufanya ufupisho huna budi kuzingatia mambo yafuatayo.

Kusoma habari uliyopewa kwa makini ili kuielewa kwa usahihi itasaidia katika kudondoa mawazo yaliyojitokeza katika habari

Kudondoa mawazo makuu katika habari kwa kuyapigia mstari yatakayo kusaidia wakati wa kujibu maswali yanayohusu ufahamu.

Kusoma swali kwa makini ili kuelewa kufahamu maana yake, na kuhusianisha na mawazo yaliyojitokeza.

Rudia kusoma habari hiyo mara kwa mara ili kuuelewa kuielewa zaidi na kuifanyia ufupisho.

Andika Ufupisho wa habari uliyo isoma kwa kutumia maneno yako bila kupoteza kiini cha habari ya awali na mara nyingi habari huwa ni theruthi ya habari ya awali


Hivyo ufupisho ni muhimu sana katika habari kwani hutumika katika shughuli mbalimbali mfano katika uhariri wa habari, kuandika ripoti ya kumbukumbu za mkutano, kudondoa mawazo makuu katika mhadhala.

**Kielelezo 11.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kueleza mambo matano ya kuzingatia wakati wa kufupisha habari kwa usahihi.

### 2.2.2 Swali la 12: Utungaji

Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji* na lililenga kupima maarifa ya watahiniwa juu ya utungaji. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua sehemu nne za utungaji wa risala.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 56.7 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Asilimia 99.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 12 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati Namba 12**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 52.3 ya watahiniwa walijibu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15 kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utungaji wa risala. Kutokana na maarifa hayo waliweza kufafanua sehemu nne za utungaji wa risala ambazo ni *kichwa cha habari/risala, utangulizi, kiini cha habari/risala na hitimisho*. Pia, watahiniwa hawa walifuata hatua zote za uandishi wa insha yaani utangulizi unaohusiana na swali, kiini na hitimisho. Kielelezo 12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

**Kielelezo 12.1**

12 Risala ni habari inayosomwa kwa
mgeni Rasmi kwa ajili ya kueleza shi
da mbalimbali au changamoto zinazo-
wakumba wasomaji risala; maranyingi
Risala husaidia watu kueleza shida
zao na mawazo yao yasikilizwe na
Mgeni waliyemwalika katika tukio
fulani; Risala huandikwa Maranyi
ngi Mashuleni wanafunzi wanapo
hitimu Masomo yao, Huandikwa kw
a wageni Maalumu walioalikwa-
kwenye tafrija tofautitofauti. Zifu
atazo ni sehemu za utungaji-
wa Risala ambazo ni;
Kichwa cha Risala; hiki ni-
Kichwa ambacho hueleza risala-
inahusu nini, kwa mfano unapotaka
kuandika risala ya ~~wahitt~~ inayo
husu Mahafali katika kichwa-
cha risala kitaandikwa kwamba
labda "RISALA YA WAHITIMU WA CHUO
CHA UALIMU KIDUGALA" kwa hiyo kich
wa hicho ndicho kinachoelezwa-
kuwa katika kichwa hiko wanao
elezewa ni wahitimu wa chuo cha
ualimu;
Utangulizi; Hapa hueleza kwa
mba kwa maamkizi mbalimbali,
kutoka kwa mgeni rasmi na wageni
wengine waliokuja kuhudhuria-
katika matukio au tukio hilo
lililompeleka na kuwakaribisha wa

12 wageni hao kwa salamu. Kwa mfa
no ndugu mgeni rasmi, mabibi na mabw
ana, walimu wa sekondari, wakufunzi
diwani wa kata, mratibu elimu kata
bwana yesu asifiwe, asalam alekumn

Kiini cha Risala; hapa kati
ka kiini cha risala ndo panapoelezw
a kwamba wanamatatizo gani kati
ka chuo chao au changamoto zinazo
wakabili, mafanikio waliyoyapata -
katika chuo hiko na mapendekezo
wanayoyatoa kutokana na changamo
to tajwa hapo ili mgeni waliomwa
lika aweze kuzitatua;

Hitimisho la Risala; Lakini
Mwisho kabisa kunakuhitimisha -
Risala hiyo kwa kumpongeza -
mgeni rasmi kuja kuungana -
nao katika Mahafali yao na
kumtaka kero ziliozotajwa ziweze
kutatuliwa;

Risala husaidia sana watu
kuwasilisha Mawazo yao katika
kifungu cha habari japokuwa kero
zinazo tajwa huwa hazitekelezw
i kwa wakati;

**Kielelezo 12.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua kwa usahihi sehemu nne za utungaji wa risala.

Asilimia 44.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hawa walishindwa kueleza kikamilifu sehemu nne za utungaji wa risala. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walitaja hatua moja wengine mbili na wengine walishindwa kufuata kanuni za uandishi wa insha.

Vilevile, asilimia ndogo ambayo ni 3.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa hawa walishindwa kueleza hatua nne za risala kwa sababu hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Utungaji* pamoja na kutokuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi yao walifafanua maeneo ambayo risala huweza kusomwa kama vile *sehemu za shuleni, hospitali, sehemu zenye shughuli maalum za kitaifa na sehemu zenye mikutano mbalimbali* badala ya *sehemu nne za utungaji wa risala ambazo ni kichwa cha habari/risala, utangulizi, kiini cha habari/risala*

*na hitimisho*. Kielelezo 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kujibu kinyume na matakwa ya swali.


**Kielelezo 12.2**

12. Utungaji wa risala ni kitendo cha kuweza
kuandaa jambo fulani ili liweze kusomwa mbele ya
mtu fulani ambaye anakuwa ameandaliwa rasmi. Hii
ina maana kwamba ni uandaaji wa taarifa ambayo
inasomwa kwa mgeni rasmi aliyehudhuria. Katika shughuli
fulani katika sehemu fulani mfano shuleni, vyuoni, kwen
ye mikutano mbalimbali ambayo inakuwa na shughuli
maalumu ambayo inakuwa imeandaliwa kwa muda maa
lumu mfano katika kipindi cha kuhitimu mafunzo ya kozi
mbalimbali. Zifuatazo ni sehemu za utungaji wa
risala.

Risala huweza kutungwa katika sehemu za shuleni
. Hii ina maana kwamba pindi wanafunzi wanapohitimu
kozi fulani ya mafunzo huweza kuagwa kwa kufanyiwa
sherehe na sherehe hiyo huweza kuandaliwa mtu au mgeni
rasmi ambaye anakuwa amealikwa hivyo huweza kuan
daliwa risala ambayo mgeni rasmi huyo huwa inamlenga
ili aweze kuitolea ufafanuzi.

Risala huweza kuandaliwa katika sehemu za hospita
li. Hii ina maana kwamba risala huweza kuandaliwa hospi
talini pindi mkuu wa wizara ya afya anapohudhuria
katika shughuli maalumu hospitali ili kuweza kujua
ni mafanikio gani yamepatikana na mapungufu yapi
yanatakiwa kutatuliwa.

Risala huweza kuandaliwa sehemu zenye shughuli
maalumu ya kitaifa ambapo Raisi anakuwa anahudhuli
a au waziri mkuu. Hii ina maana kwamba risala huwe
za kuandaliwa katika sehemu zenye maadhimisho
maalumu ya kitaifa ambayo yanahudhuriwa na
viongozi wa ngazi za juu wa serikali ili kuweza
kujua mapungufu na mafanikio ambayo yanakuwa
yamefanyika kwa kipindi fulani.



12. Risala huweza Kuandaliwa Katika Sehemu za mikutano mbalimbali. Hii ina maana kwambo risala huweza Kuandaliwa Katika sehemu zenye mikutano mbalimbali ambapo viongozi kama mbunge, diwani, Mwenyekiti wa Kijiji huweza Kuwakilisha viongozi wa juu wa Serikali.


Hivyo basi risala huweza Kutungwa Katika Sehemu hizi ambazo zinakuwa shughuli fulani ambayo inakuwa na umuhimu Katika Kufanikisha jambo fulani.

**Kielelezo 12.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua maeneo ambayo risala huweza kusomwa badala ya sehemu nne za utungaji wa risala.

### 2.2.3 Swali la 13: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lilimtaka mtahiniwa abainishe manufaa matano ya vitendawili katika jamii.

Idadi ya watahiniwa waliojibu swali hili ni sawa na asilimia 91.9 kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Asilimia 98.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 13 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.






**Chati Namba 13**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Aidha, asilimia 55.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Baadhi yao walitoa hoja ambazo hazikufika tano na wengine walikosa alama za utangulizi na hitimisho kwa sababu hawakujibu swali hili kwa mfumo wa insha.

Hali kadhalika, asilimia 42.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hawa waliweza kubainisha manufaa ya vitendawili ambayo ni *kudumisha mila na desturi, kuburudisha jamii husika, hukuza fikra za watumiaji, huelimisha jamii na hukuza lugha kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa insha*. Licha ya kubainisha manufaa ya vitendawili kwa usahihi, baadhi ya watahiniwa waliweza kuandika utangulizi wa insha unaojitosheleza na hitimisho zuri linaloendana na swali. Kielelezo 13.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri.

**Kielelezo 13.1**


12. Vitendawili ni aina ya semi inayotumia
lugha ya picha au lugha ~~paba~~ mafumbo ~~bapa~~ ili
kufikisha ujumbe na mala nyingi hutumia
Maana iliyojificha. hivyo ni lazima uweze
kufumbua fumbo husika ndipo uweze kuelewa.
Vitendawili vinaumuhimu mkubwa sana katika
jamii. yafuatayo ni baadhi ya manufaa ya vitendawili kwa jamii
Kudumisha mila na desturi ya jamii au
Kutunza amari za jamii. Vitendawili vinahusisha
Mambo ya kale yaliyotokea katika jamii husika
hivyo basi kupitia kutega na kutegua kitendawili
tamaduni zile na mila huweza kuenea
kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
Kuonya jamii husika; kwa mfano
Kitendawili kama vile dua la kuku ~~mwewe~~ halimpati
Mwewe, huonya kuwa kumuombea mtu mabaya si jambo
jema maana apangaye ni mungu
Kuburudisha Jamii; Vitendawili




13. pia huweza kuburudisha jamii husika kwa mfano babu anaweza kukaa na wajukuu zake na kuanza kutegeana vitendawili na kutegua hivyo kuwafanya waclolee na kufurahi pamoja hivyo kufanya jamii hiyo kuburudika.
Kukuza lugha katika jamii husika; pia vitendawili vinaweza kupelekea lugha ya jamii fulani kukua kutokana na baadhi ya maneno yanayotumika katika vitendawili kuweza kuingia moja kwa moja katika lugha ya jamii husika.
Kuelimisha jamii husika; kwa kutumia vitendawili jamii inaweza kuelimika kutokana na mafunzo mbalimbali yanayopatikana katika vitendawili.
Kuvuta usikivu wa jamii; Pia vitendawili huweza kutumika kuvuta usikivu miongoni mwa jamii, kwa mfano katika mikutano mbalimbali endapo watu wanapiga kelele au wamechoka kusikiliza unaweza kutega na kutegua vitendawili na kuwafanya watu wakufuatilie kwa makini na hivyo kuvuta usikivu.
Kumfikirisha mtu; Pia vitendawili vinaweza kumfanya mtu afikirie kwa makini pale anapoambia ategue kitendawili kilichotegwa.
Kwa ujumla vitendawili ni muhimu sana kwa jamii husika katika kufanikisha mambo mbalimbali kama vile kutambulisha jamii fulani na kuweza kutoa mafunzo mbalimbali kupitia vitendawili hivyo.

**Kielelezo 13.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha vizuri manufaa ya vitendawili katika jamii.

Vilevile, watahiniwa wachache sana ambao ni asilimia 1.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa hawa walipata alama hafifu kwa sababu baadhi yao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ndogo ya *Vitendawili*, wengine walichanganya sifa za vitendawili na manufaa ya vitendawili na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walikosa alama za,

utangulizi, kuelezea hoja na hitimisho kwa sababu walijibu swali kwa mfumo wa kuorodhesha hoja badala ya insha. Kielelezo 13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kushindwa kutimiza matakwa ya swali.

**Kielelezo 13.2**


13. Manufaa ya vitendawili katika jamii
i. Hukarca jamii
ii Huelimisha jamii
iii Huonya jamii
iv. Hufichia mambo maovu
v. Hukemea maovu.


**Kielelezo 13.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeorodhesha manufaa ya vitendawili badala ya kuandika insha. Hata hivyo, amerudia rudia baadhi ya hoja kama hoja namba iii na v.

## 2.3 SEHEMU C: MASWALI YA INSHA YANAYOHUSU MADA ZA UFUNDISHAJI

### 2.3.1 Swali la 14: Upimaji.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Upimaji* ambapo lilimtaka mtahiniwa kubainisha faida tano za upimaji wa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Watahiniwa waliojibu swali hili ni asilimia 69.6 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Asilimia 99.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifanya vizuri na kupata alama za wastani na zaidi. Watahiniwa hawa waliweza kubainisha faida tano za upimaji wa wanafunzi. Chati namba 14 inaonesha viwango vya kufaulu katika asilimia.




**Chati Namba 14**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 84.6 walifanya vizuri na kupata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hawa walifanya vizuri kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Upimaji* , waliweza kuzingatia matakwa ya swali na kanuni za uandishi wa insha. Baadhi yao waliweza kubainisha kwa usahihi faida tano za upimaji wa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Faida walizobainisha ni pamoja na *kumsaidia mwalimu kujua kiwango cha uelewa cha wanafunzi, kuboresha mbinu na zana za kufundishia, kujua maendeleo ya wanafunzi wao, kutatua matatizo mbalimbali ya wanafunzi na kutathmini ufundishaji*. Kielelezo 14.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu.

**Kielelezo 14.1**

14 Upimaji – Ni kitendo cha kuchunguza ni kwa kiasi gani maarifa yaliyotolewa kwa wanafunzi yameeleweka. Upimaji huweza kufanyika kwa kutumia majaribio, mtihani, orodha hakiki, mkoba wa kazi na maswali dodoso. Upimaji wa wanafunzi una faida kubwa sana katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwani unasaidia katika:

Humsaidia mwalimu kujua kiwango cha uelewa wa wanafunzi wake darasani. Kupitia upimaji wa wanafunzi mwalimu huweza kujua kiwango cha uelewa wa wanafunzi kwani upimaji humsaidia mwalimu kutambua wanafunzi ambao kiwango au uelewa wao darasani ni mdogo na pia kuwatambua wale wenye uelewa wa haraka

Humsaidia mwalimu kuboresha mbinu na zana za kufundishia na kujifunzia. Pia upimaji humsaidia mwalimu katika uboreshaji wa mbinu na zana za ufundishaji na ujifunzaji pale wanafunzi wanapofeli sana mwalimu huweza kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wake mfano kama alikuwa anatumia mbinu moja katika ufundishaji na ujifunzaji huweza kuamua kutumia mbinu zaidi ya moja ili wanafunzi waweze kuelewa.

Huwasaidia wazazi kujua maendeleo ya watoto wao. Pia upimaji wa wanafunzi una faida kwani matokeo ya upimaji huwasaidia wazazi kujua maendeleo ya

14. watoto wao kitaaluma shuleni kama ni mabaya au mazuri hivyo kuwasaidia katika kufanya maamuzi juu ya mtoto kama ni kumpongeza au kumhimiza aongeze bidii katika masomo.

Humsaidia mwalimu kutathmini ufundishaji wake darasani, pia upimaji wa wanafunzi humsaidia mwalimu kutathmini ufanisi wake katika kufundisha somo husika hivyo kuweza kufanya maamuzi juu ya mchakato wa ufundishaji wake kama ni mzuri au mbaya na hivyo kuamua ni nini cha kufanya ili aweze kurekebisha au kuboresha zaidi

Husaidia katika kutatua matatizo mbalimbali ya wanafunzi, pia kupitia upimaji mwalimu huweza kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili wanafunzi wake mfano athari za lugha mama, pia matatizo mengine ambayo yanaathiri ujifunzaji wa mwanafunzi. Hivyo kupitia upimaji wa mwanafunzi mwalimu huweza kumsaidia mwanafunzi huyo kwa kumpa njia au mbinu za kukabiliana na changamoto zinazomkabili


Upimaji katika Tasnia ya Elimu ni muhimu sana kwani una umuhimu mkubwa kwa mwalimu na mwanafunzi hivyo ni muhimu mwalimu kuhakikisha kuwa anawapima wanafunzi wake pia bila upimaji wanafunzi hawawezi kuendelea katika ngazi nyingine za Elimu kwani matokeo ya upimaji ndio tiketi ya kuendelea mbele

**Kielelezo 14.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha vizuri faida tano za upimaji wa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Aidha, asilimia 15 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Upimaji* na pia hawakuzingatia matakwa ya swali kama vile kujibu swali kwa mfumo wa insha.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sana ambao ni asilimia 0.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa juu ya mada ya upimaji. Baadhi yao waliandika majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 14.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kukosa uelewa wa kutosha juu ya faida za upimaji wa wanafunzi.

**Kielelezo 14.2**



14. Upimaji
Hili ni tendo la kukupima ili kujua ni vipi au namna gani unaendelea katika zoezi la ujifunzaji na ufundishaji, Zifuatazo ni faida tano katika zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji.
Zoezi Upimaji katika ufundishaji na kujifunzaji linatusaidia katika kupata uzoefu wa kufundisha wanafunzi na pia tunaweza kusimama mbele za wanafunzi na kufundisha bila kubabaika.
Pia hutujengea kujiamini, kwani unaweza kusimama mbele ya wanafunzi na kufundisha somo fulani bila ya kujingatangata au kutetemeka kwa aina yoyote.
Kujenga kumbukumbu, ili zoezi la upimaji usaidia saidia sana katika kujenga kumbukumbu si rahisi kusahau mambo uliyojifunza na mambo uliofundisha kwa kipindi kirefu au kwa kipindi cha muda fulani.
Katika ufaulu pia upimaji katika mchakato wa ujifunzaji au ufundishaji husaidia sana si rahisi kusahau, pia unaweza kujibia maswali baada ya kukumbuka kile ulichokisoma au ulichojifunza kwa muda fulani.

**Kielelezo 14.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali.

### 2.3.2 Swali la 15: Zana za Kufundishia na Kujifunzia Soma la Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuchambua mambo matano ya kuzingatia wakati wa kutayarisha zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 52.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi na watahiniwa wengi. Asilimia 99.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu na za wastani. Chati namba 15 inaonesha kiwango cha kufaulu katika asilimia.





**Chati Namba 15**: Kufaulu kwa Watahiniwa Kwa Asilimia

Asilimia 54.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri na kupata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Baadhi yao waliweza kuchambua kwa usahihi mambo ya kuzingatia katika uandaaji wa zana za kufundishia na kujifunzia. Miongoni mwa mambo waliyoyachambua ni pamoja na *malengo mahsusi ya somo, umri na uelewa wa wanafunzi, zana zinazowafikirisha wanafunzi, ukubwa wa zana unaoendana na ukubwa wa darasa na iwe bora na imara*. Pia, waliweza kuzingatia taratibu za uandishi wa insha kama vile kuanza kwa utangulizi wa swali, kiini na hitimisho. Pia, baadhi yao walizingatia matumizi mazuri ya lugha na mtiririko mzuri wa hoja wenye mantiki. Kielelezo 15.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu.

**Kielelzo 15.1**

15. Zana za Kufundishia Ni kitu chochote
Kinachorahisisha tendo la Ujifunzaji na Ufundi
shaji darasani. Yapo Mambo ya Kuzingatia waka
ti wa Kutayarisha zana za Kufundishia na
Kujifunzia Katika Somo la Kiswahili. Yafuatayo
ni Mambo ya Kuzingatia wakati wa Kutayarisha
Zana za Kufundishia na Kujifunzia.
Zana Iendane na Malengo Mahususi ya Somo;
Miongoni Mwa Mambo Muhimu ya Kuzingatiwa wa-
kati wa Kuandaa zana ni Muhimu Zana ya Kufund
ishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili Iendane na
Malengo Mahususi ya Somo. Kama Zana haiendani
na Malengo Mahususi ya Somo Wanafunzi hawawezi
Kuelewa Somo Kutokana na Kutoingiliana kwa Ma
arifa ya Zana na Malengo Mahususi ya Somo.
Zana Iendane na Umri na Uelewa wa Mwa
nafunzi; Ni Muhimu zana Inapotayarishwa Izing
atie Umri na Uelewa wa Mwanafunzi yaani Ma
arifa yanayotolewa yawe yanaendana na Umri
wa Mwanafunzi Ili Kufanikisha tendo la Ufu
ndishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili.
Zana Iwe Inamfikilisha Mwanafunzi; Zana
bora ni Ile Inayomfikilisha Mwanafunzi Ili
aweze Kujenga Kumbukumbu ya Kudumu Kuto
kana na Zana hiyo. Hivyo katika Utayarishaji
wa Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo
la Kiswahili ni Muhimu Kuzingatia Kutayarisha
Zana Inayomfikilisha Mwanafunzi.
Zana Iwe bora na Imara; Ili zana
Iweze Kutumika Vizuri na Kwa Urahisi ni
Muhimu zana Iwe bora na Imara. Ili Iweze
Kutumika Vizuri Kurahisisha Tendo la Ufundishaji


15. na Ujifunzaji wa somo la Kiswahili.
Zana Iwe na Ukubwa Unaofaa. Kulingana na Idadi ya Wanafunzi, Ili Wanafunzi wote da rasani Waweze Kushiriki Kikamilifu katika somo la Kiswahili ni Muhimu Zana Inayotumika Iwe na Ukubwa Unaofaa. Na Ukubwa huo hutoka na na Idadi ya Wanafunzi waliopo darasani.
Hivyo basi Mambo Muhimu ya Kuzingatia wakati wa Kutayarisha zana za Kufundishia na Kujifunzia somo la Kiswahili ni hizo. Ili Kuboresha vitendo vya Ufundishaji na Ujifunz aji Ni Muhimu Kufuata hatua za Uandaaji Zana bora.

**Kielelezo 15.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyechambua vizuri mambo matano ya kuzingatia wakati wa utayarishaji wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

Asilimia 44.9 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hawa walipata alama za wastani kwa sababu walichanganya mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia Kiswahili na hatua za kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

Aidha, asilimia 0.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5 kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya uandaaji wa zana za kufundishia na kujifunzia pamoja na kutokuelewa matakwa ya swali. Baadhi yao waliandika vifaa vya maandalizi ya kufundishia badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa kutayarisha zana za kufundishia na kujifunzia. Vifaa vya maandalizi ya kufundishia vilivyobainishwa na watahiniwa hawa ni kama vile *azimio la kazi, andalio la somo, shajara la somo na nukuu za somo* badala ya mambo ya kuzingatia katika uandaaji wa zana za kufundishia na kujifunzia ambayo ni *malengo mahsusi ya somo, umri na uelewa wa wanafunzi, zana zinazowafikirisha wanafunzi, ukubwa wa zana unaoendana na ukubwa wa darasa na iwe bora na imara*. Kielelezo 15.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuchambua mambo ya kuzingatia katika uandaaji wa zana za kufundishia na kujifunzia.

**Kielelezo 15.2**

15. Zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili ni nyenzo au vifaa maalumu vinavyoandaliwa na mwalimu wa somo au mtu mwingine katika kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili darasani.

Mambo matano (5) ya kuzingatia wakati wa kutayarisha zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili ni kama yafuatayo.

15. Maandalizi (Utayarishaji) Ya Azimio La Kazi: Azimio la Kazi ni mpango mzima unaoandaliwa na mwalimu wa somo la Kiswahili katika kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo kwa muhula mmoja au mwaka mzima. Azimio la kazi linatokana na muhtasari wa somo la Kiswahili.

Maandalizi (Utayarishaji) Ya Andalio la Somo: Andalio la Somo ni mpango ambao mwalimu wa somo huuandaa kabla [illegible] ya kwenda kufundisha somo lake. Maandalizi haya huwa yanafanyika kila siku kabla ya kuingia darasani.

Maandalizi Ya Kisaikolojia: Haya ni maandalizi yanayohusu tabia, ubongo na fikra zilizomo ndani ya binadamu.

Maandalizi ya Shajara ya Somo: Shajara ya somo ni daftari au mkoba au jalada linaloandaliwa rasmi kwa ajili ya kuhifadhi rekodi za mada na mada ndogo ndogo zilizofundishwa na mwalimu darasani.

Maandalizi Ya Nukuu za Somo: Nukuu ni vyanzo mbalimbali (tofauti) zinazopatikana katika gazeti, mtandaoni, majarida, vitabu na kuendelea.


Utayarishaji wa Zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili, ni vizuri [illegible] uzingatiwe [illegible] [illegible] kurahisisha mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

**Kielelezo 15.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika vifaa muhimu vya maandalizi ya kufundishia badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa kutayarisha zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

### 2.3.3 Swali la 16: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya *Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili*. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua manufaa matano ya muhtasari kwa mwalimu wa somo la Kiswahili.

Watahiniwa waliofanya swali hili ni asilimia 75 kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani wa Kiswahili na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 99.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri na kupata alama za wastani na zaidi. Chati namba 16 inaonesha kiwango cha kufaulu kiasilimia.




**Chati Namba 16**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 79.1 walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili* hivyo waliweza kufafanua kwa usahihi manufaa matano ya muhtasari ambayo ni *humsaidia mwalimu katika kuandaa azimio la kazi, kujua mbinu za kufundishia, kujua zana za kufundishia mada husika, kujua malengo yanayotakiwa kufikiwa na kujua idadi ya vipindi kwa kila mada*. Pia, watahiniwa wa kundi hili walizingatia taratibu za uandishi wa insha. Kielelezo 16.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu.

**Kielelezo 16.1**

16 Muhtasari ni ufupisho wa maudhui au mada ambazo zipo katika kitabu cha kiada cha Somo la kiswahili. Muhtasari umebeba mada zote ambazo mwanafunzi anapaswa kufundishwa katika kipindi chake chote cha mafunzo. Muhtasari una manufaa mengi kwa mwalimu yafuatayo ni manufaa hayo

Humsaidia mwalimu katika uandaaji wa azimio la kazi. Mwalimu anapoandaa mpango kazi wake wa muda mrefu hutumia muhtasari, Muhtasari humsaidia katika uchambuzi wa vitu mbalimbali au vipengele mbalimbali mfano kuchambua vipindi ambavyo atatumia katika kufundishia mada za Somo la kiswahili

Humsaidia mwalimu kujua mbinu za kufundishia Somo la kiswahili, Mwalimu anapotumia muhtasari wa Somo la kiswahili huweza kutambua ni mbinu gani ambazo atatumia katika kufanikisha upatikanaji wa maarifa kwa mwanafunzi unakuwa ni wenye ufanisi. Pia mwalimu huweza kutambua ni gani mwanafunzi atajifunzia.

Humsaidia mwalimu kujua zana zipi anapaswa kutumia katika kila mada ya Somo la kiswahili, Zana huweza kumsaidia mwalimu kufundisha Somo lake kwa urahisi ambapo inamsaidia kutumia muda mchache katika kueleza dhana mbalimbali pia inamsaidia katika kueleza dhana tata za Somo la kiswahili.

16 Humsaidia mwalimu kujua ni malengo ya-
pi yanatakiwa kufikiwa. Katika muhtasari huwe-
za kuelezea malengo ya kila mada ambayo
mwalimu wa somo la kiswahili anatakiwa ay-
afikie katika kipindi fulani ambacho kime
pangwa
Kujua idadi ya vipindi. Mwalimu a
napo chambua muhtasari huweza kutambua idadi
ya ~~kila~~ ~~kipin~~ mada ndogo na kila mada na vi
pindi vyake hivyo humsaidia kuandaa ma
da zake ~~kwo~~ kuzingatia idadi ya vipindi
kwa kila mada na humsaidia kufundisha somo
lake la kiswahili kwa wakati ambao umepa
ngwa
Hitimisho: Muhtasari una manufaa me
ngi si hayo tu bali pia humsaidia mwalimu ku
jua ujuzi ambao anatakiwa aufikishe pamoja na
kujua mtiririko wa mada..

**Kielelezo 16.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi manufaa matano ya muhtasari kwa mwalimu wa somo la Kiswahili.

Aidha, asilimia 20.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kati ya 6 hadi 10. Baadhi yao walishindwa kutimiza matakwa ya swali, wengine walishindwa kufuata kanuni na taratibu za uandishi wa insha na wengine walishindwa kupanga hoja zao katika mtiririko unaoleta mantiki. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walikosa alama za utangulizi, kueleza hoja, na hitimisho kwa sababu walijibu swali kwa mtindo wa kuorodhesha hoja badala ya kuandika insha.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sana sawa na asilimia 0.1 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya manufaa ya muhtasari kwa mwalimu wa somo la Kiswahili. Baadhi yao walishindwa kufafanua kikamilifu manufaa matano ya muhtasari kwa mwalimu wa somo la Kiswahili. Kielelezo 16.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua manufaa ya muhtasari wa somo la Kiswahili na kupata alama hafifu.

**Kielelezo 16. 2**

16. Muhtasari ni Ufupisho wa maudhui. ~~yate~~ hivyo basi kuna manufaa ya muhtasari kwa mwalimu wa somo la Kiswahili. nazo ni kama-zifuatazo.

Humwelekeze mwalimu njia au mbinu za-kutumia katika kufundisha, hivyo basi mwalimu-anakuwa anajua njia za kutumia wakati wakufu-ndisha.

Muhtasari huonyesha mada kuu ~~na~~ mada ndogo zote kwa mtiririko uliyosahihi, mwalimu hapo anakuwa-tayari anajua ni jinsi gani atatumia mada kuu na mada ndogo ipasavyo.

Muhtasari humwelekeza mwalimu wa Kiswahili jinsi ya kuazimia na kuandalia kwa mtiririko unaofaa.

Huonyesha kalenda ya shule jinsi ya kujua idadi ya vipindi alivyo navyo mwalimu au ana-takiwa kufundisha vipindi vingapi fote hayo ~~tna~~ yaratokana na muhtasari.

Muhtasari humrahisishia mwalimu kazi kwani mada zote zinakuwa zimesha-mbuliwa,

Hivyo basi hayo ndiyo manufaa ya ~~mtasaai~~ muhtasari kwa mwalimu wa Kiswahili kwani muhtasari humwonyesha aina ya zana anayotakiwa kutumia ~~wate~~ kwa kila mada.

**Kielelezo 16.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua kikamilifu manufaa matano ya muhtasari kwa mwalimu wa somo la Kiswahili. Hata hivyo, miongoni mwa hoja alizoandika ni hoja moja tu katika aya ya tatu inayohusu manufaa ya muhtasari kwa mwalimu wa somo la Kiswahili.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa 621 Kiswahili ulikuwa na maswali (16) yaliyotoka katika mada ya *Stadi za Lugha, Fasihi Simulizi, Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili, Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Kiswahili, Utungaji, Sarufi, Upimaji, Ufahamu* na *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*.

Uchambuzi wa kufaulu kwa watahiniwa katika mada hizo unaonesha kuwa watahiniwa wamefanya vizuri katika mada 7 ambazo ni sawa na asilimia 77.8 ya mada zilizotahiniwa. Mada hizo ni *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili* (99.6%), *Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Kiswahili* (99%), *Fasihi Simulizi* (90.8%), *Utungaji* (85%), *Upimaji* (80.8%), *Stadi za Lugha* (80.5%), na *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili* (77.5%).

Aidha, wanafunzi walipata kiwango cha kufaulu cha wastani katika mada 2 ambazo ni sawa na asilimia 22.2 ya mada zilizotahiniwa. Mada hizo ni *Sarufi* (*62%)* na *Ufahamu* (62.4%).

Watahiniwa walipata kiwango kizuri cha kufaulu katika mada zilizotajwa kutokana na uelewa wa kutosha wa mada zilizotahiniwa na utambuzi sahihi wa matakwa ya kila swali. Hata hivyo, wengi wao waliweza kujieleza vizuri kwa lugha inayoeleweka, kujenga hoja vizuri katika mtiririko unaoleta mantiki pamoja na kufuata taratibu na kanuni za uandishi hasa katika maswali ya insha.

Hata hivyo, watahiniwa walipata kiwango cha wastani cha kufaulu katika mada zilizotajwa kutokana na uelewa mdogo wa mada zilizotahiniwa na kutokuelewa matakwa ya swali. Mchanganuo wa kufaulu kwa watahiniwa kwa mada umefafanuliwa katika viambatisho A na B.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kwa mada ni asilimia 81.1. Hali hii inaonesha kuwa zaidi ya 2/3 ya watahiniwa walikuwa na uelewa mzuri wa mada mbalimbali zilizotahiniwa.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, mtihani wa Ualimu Daraja la A katika somo la Kiswahili mwaka 2018 ulizingatia Muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya utambuzi yaani maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kilikuwa ni kizuri ambapo wastani wa kufaulu wa somo hili ni asilimia 84.1.

Hata hivyo, uchambuzi huu umebaini changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa. Changamoto hizo ni pamoja na uelewa mdogo katika mada mbalimbali kama vile mada ya *Sarufi* na *Ufahamu* ambao umewafanya watahiniwa washindwe kuelewa matakwa ya swali. Pia, changamoto nyingine ni baadhi ya watahiniwa kutokuwa na ujuzi wa kujieleza kwa ufasaha hasa katika kujenga hoja zenye mtiririko wenye mantiki. Hali kadhalika, changamoto nyingine ni watahiniwa kutokufuata maelekezo ya mtihani. Kwa mfano, maswali yaliyowataka kujibu kwa mtindo wa insha baadhi yao walijibu kwa mtindo wa kuorodhesha hoja.

Mwisho, inatarajiwa kuwa taarifa hii ya uchambuzi kuhusu majibu ya watahiniwa itasaidia kuinua kiwango cha kufaulu cha somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa mafunzo ya Ualimu Daraja la A. Aidha, taarifa hii itawasaidia walimu tarajali na wakufunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali kwa kuona makosa yaliyosababisha kiwango hafifu cha kufaulu na kufanya marekebisho ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa wa somo la Kiswahili inapendekezwa kuwa:

(a) Walimu tarajali wafundishwe na wasisitizwe kuzingatia kanuni na taratibu za uandishi hasa matumizi sahihi ya alama za uandishi, kanuni za kisarufi pamoja na ujenzi mzuri wa hoja wenye mtiririko unaoleta mantiki.

(b) Wakufunzi na walimu tarajali wazingatie ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote zilizoko katika Muhtasari wa somo hili kwa ukamilifu wake.

(c) Wakufunzi wanasisitizwa kutumia mbinu na zana anuwai katika kufundisha mada za *Sarufi* na *Ufahamu* kama zilivyoainishwa kwenye muhtasari wa somo.

(d) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia chini ya Idara ya Ualimu iandae semina elekezi kwa wakufunzi wa somo la Kiswahili katika mada za sarufi hususan *Aina za Maneno*, hii itasaidia wakufunzi kubadilishana ujuzi juu ya dhana walizonazo zinazohusu mada hiyo ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika somo hili.

**KIAMBATISHO A**


## UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

| NA | Mada | Namba ya Swali | Viwango vya Kufaulu (%) | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Asilimia 40 na zaidi | Wastani | |
| 1 | Zana za Kufundishia na Kufundishia Somo la Kiswahili | 15 | 99.6 | 99.6 | Vizuri |
| 2 | Maandalizi ya Ufundishaji | 6 | 98 | 99 | Vizuri |
| | | 16 | 99.9 | | |
| 3 | Fasihi Simulizi | 2 | 82.9 | 90.8 | Vizuri |
| | | 5 | 90.8 | | |
| | | 13 | 98.8 | | |
| 4 | Utungaji | 7 | 70.8 | 85 | Vizuri |
| | | 12 | 99.2 | | |
| 5 | Upimaji | 9 | 62 | 80.8 | Vizuri |
| | | 14 | 99.6 | | |
| 6 | Stadi za Lugha | 1 | 78.1 | 80.5 | Vizuri |
| | | 3 | 83.6 | | |
| 7 | Mbinu za kufundishia na kujifunzia Kiswahili | 4 | 75.7 | 77.5 | Vizuri |
| | | 10 | 79.2 | | |
| 8 | Ufahamu | 11 | 62.4 | 62.4 | Wastani |
| 9 | Sarufi | 8 | 62 | 62 | Wastani |

**KIAMBATISHO B**

## UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

## 621 KISWAHILI - 2018



cmyk